**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 12 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, karibuni sana Dodoma. Natanguliza tangazo moja la muhimu kwamba mtambo wa kuzuia simu zisiite ama zisipokelewe haufanyi kazi leo asubuhi. Kwa hiyo, nawaombeni sasa hivi yeyote aliye na simu aizime ili tuweze kuendelea kwa utulivu.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OF1SI YA WAZIRI MKUU (DR. BATRIDA SALHA BURIAN):**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**MASWALI NA MAJlBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la kwanza la Mkutano na Kikao hiki cha Kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir.

**MHE. HAFlDH ALl TAHIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza katika kipindi hiki cha Bajeti kuuliza swali la kwanza. Lakini nasikitika kwa sababu zisizozuilika, naomba swali langu lijibiwe katika tarehe nyingine katika kipindi hicho. Ahsante.

**Na.2**

**Ubovu wa Daraja la Mto Simiyu -Bariadi**

**MHE. JOYCE N. MACHIMU** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Jimbo la Bariadi Mashariki moja ya adha zinazowakabili wananchi ni pamoja na kutojengwa kwa Daraja la Mto Simiyu licha ya ahadi ya Mheshimiwa Rais Kikwete aliyoitoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu:-

Je, katika bajeti ya mwaka 2007/2008 Serikali imetenga fedha za ujenzi wa daraja hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Machimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa kwenye kampeni za uchaguzi za mwaka 2005 alitoa ahadi ya kujenga daraja katika Mto Simiyu uliopo mpakani mwa Wilaya za Meatu na Bariadi. Katika utekelezaji wa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais, Serikali ilitenga shilingi milioni 229 katika mwaka wa fedha 2006/2007 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa mita 50. Hadi kufikia mwezi Mei, mwaka huu fedha hizo zote zilipelekwa na kupokelewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mvua nyingi zilizokuwa zikinyesha na Mto Simiyu kujaa maji, hapakuweza kufanyika kazi yoyote ya ujenzi wa daraja hadi maji yatakapopungua.

Halmashauri ya Wilaya ya Meatu imeingia mkataba na Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Shinyanga kuwa msimamizi mshauri wa ujenzi wa daraja hilo. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 23 kati ya fedha zilizotolewa zimetumika kulipia gharama za usanifu pia usimamizi wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi atakayefanya kazi ya ujenzi wa daraja hilo umeanza kwa kutangaza zabuni tarehe 14/05/2007. Ufunguzi wa zabuni unafanyika leo hii. Mara tu baada ya ufunguzi, itafanyika tathimini ya zabuni na mkandarasi atakayeshinda atakabidhiwa kazi hiyo. Kazi ya ujenzi wa daraja la mto Simiyu inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba mwaka huu 2007.

**Na.3**

**Malipo kwa Watumishi Waliotibu Wagonjwa wa Kipindupindu Hospitali ya Mkoa Kigoma**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE (k.n.y. MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa ugonjwa wa kipindupindu mwaka 2000-2001 wapo wafanyakazi waliotibu wagonjwa wa kipindupindu ambapo baadhi walilipwa na wengine hawakulipwa:-

Je, Serikali inasemaje juu ya malipo ya watumishi ambao hawakulipwa fedha zao katika hospitali ya Mkoa wa Kigoma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ulitokea mlipuko wa Ugonjwa wa Kipindupindu kwa mwaka 2000-2001 katika Mji wa Kigoma na katika Halmashauri nyingine katika Mji wa Kigoma. Katika mchakato wa kuandaa malipo, jumla ya watumishi 169 waliohudumia wagonjwa kutoka Halmashauri zote nne Mkoani Kigoma walileta madai yao kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Watumishi 25 walihudumia wagonjwa; Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji, Watumishi 25 walihudumia wagonjwa hawa; Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Watumishi 37 na Hospitali ya Mkoa, Watumishi 60 ndiyo waliofanya kazi ya kuhudumia hawa wagonjwa wa kipindupindu.

Mheshimiwa Spika, jumla ya madai yote yaliyowasilishwa ni Sh. 22,728,000/=. Baada ya kufanyiwa uhakiki, madai halali yalionekana ni shilingi milioni 16.7. Kwa kuwa gharama za magonjwa ya milipuko hutolewa na Wizara ya Fedha, madai hayo yalipelekwa Wizarani baada ya kuidhinishwa na Wizara ya Afya. Fedha zilizotolewa ni shilingi milioni 10 tu kati ya shilingi milioni 16 zilizohitajika.

Katika hospitali ya Mkoa wa Kigoma jumla ya watumishi 60 walilipwa jumla ya shilingi milioni 2.1 kama posho za kufanya kazi saa za ziada *(extra duty allowance)* wakati wa mlipuko wa ugonjwa huo; Watumishi wanane wa Kamati ya uendeshaji afya ya Mkoa; Watumishi 14 walioshughulikia wagonjwa; Watumishi 28 waliokuwa wakifanya kazi katika wodi namba 2, 5, 6, na 8 na Watumishi wanane waliokuwa wanafanya kazi katika Maabara na Madereva wawili.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baadhi ya watumishi wote walilipwa posho, lakini sio kiwango kilichotakiwa kwa sababu fedha zilizotolewa zilikuwa kidogo. Kwa hivi sasa ofisi yangu inakusanya taarifa za madai ya watumishi wa Idara ya Afya kutoka Halmashauri zote nchini. Baada ya uhakiki wa madai hayo, Serikali itakuwa katika nafasi

nzuri ya kutatua tatizo hili ikiwa ni pamoja na la watumishi wa afya Mkoani Kigoma.

**SPIKA**: Loo! Naona Waheshimiwa Wabunge sijui bado hawajaamka! Tunaendelea. *(Makofi/Kicheko)*

**Na.4**

**Utaratibu wa Safari za Watendaji wa Serikali**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZlNDAKAYA (k.n.y. MHE. JANETH M. MASSABURI)** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya watendaji wa Serikali hutumia muda mwingi na fedha nyingi kuhudhuria semina, warsha, makongamano na safari za nje zisizoleta mageuzi ya kiutendaji:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu kuratibu safari za watendaji wa Serikali kwa ngazi ya Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wa Halmashauri na Taasisi za Umma kwa kuomba kibali maalum kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya mlolongo wa warsha, semina na makongamano yanayofanyika nchi nzima ambayo huigharimu Serikali fedha nyingi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu muafaka wa kuratibu safari za Watumishi wa Serikali wakiwemo Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Halmashauri umeelezwa katika kifungu cha (3) cha Waraka wa Utumishi Na. 7 wa mwaka 2004 ambapo kiwango cha juu cha muda wa kusafiri nje ya kituo cha kazi ni siku 60 kwa mwaka wa fedha. Ki1a mtumishi anatakiwa kujaza fomu maalum kuonyesha idadi ya siku atakazokuwa nje ya ofisi. Safari hizo zitaidhinishwa na mamlaka mbalimbali za juu za utumishi katika Utumishi wa Umma. Kwa Makatibu Wakuu wataomba idhini kwa Katibu Mkuu Kiongozi; kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, kwa Wakuu wa Mikoa; kwa Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kwa Wakuu wa Wilaya husika na kwa watumishi wengine wa Umma, kwa Watendaji Wakuu wa sehemu zao za kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, ingawa ni kweli kuwa warsha, semina na makongamano, huigharimu Serikali fedha nyingi, Serikali imeweka utaratibu unaopaswa kuzingatiwa kama ulivyofafanuliwa katika Waraka wa Rais Na.l wa mwaka 1992 na Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 1998. Kama hatua za kubana matumizi, Serikali imeelekeza kuwa Mikutano, warsha, semina na makongamano vipunguzwe na kubakia ile muhimu ambayo ina mwelekeo wa kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, hata kwa semina, warsha na makongamano yatakayoonekana ni muhimu, imeelezwa kwamba yapangwe kwa namna ambayo gharama zake zitakuwa nafuu. Kwa mfano, kama washiriki wengi wako Dar es Salaam yafanyike Dar es Salaam na sio Arusha, Mwanza au mahali pengine popote yachukuliwe muda mfupi, yaani zipangwe programu ambazo zitachukua siku moja au mbili badala ya kuchukua wiki nzima bila ulazima wowote na Taasisi zitakazoalika viongozi kufunga au kufungua semina hizo zigharamie za viongozi hao.

**SPIKA**: Naam. Swali la kwanza la nyongeza la Mkutano huu linaulizwa na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, Mbunge wa Kwela.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZlNDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Je, Waziri atakubaliana nami kwamba watumishi wa Serikali wanafanya safari nyingi za nje ya nchi kuliko kwenda Mikoani na anaweza akatufafanulia gharama za safari hizo zimekuwa kiasi gani? *(Makofi)*

(b) Waziri anafahamu kwamba semina na makongomano sasa vimekuwa kero na gharama kubwa kwa nchi na baadhi ya watumishi wa Dar es Salaam kuhama majumbani kwao na kwenda kukaa katika hoteli za pale pale Dar es Salaam kufanya semina? *(Makofi)*

**SPIKA:** Katika lile swali la kwanza sehemu ya pili ya swali la kwanza 1inalotaka kujua gharama zote za safari zote za watumishi, nadhani hilo litahitaji kuulizwa kwa maandishi. Lakini yaliyobaki Waziri unaweza kujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sina takwimu ya safari za nje na za ndani za kwenda Mikoani, siwezi kukubaliana na yeye na wala siwezi kumkatalia yeye kwa kuwa sina takwimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kama nilivyosema kwamba Serikali imeelekeza kupunguza yale makongamano na semina ambazo hazina umuhimu kwa maana ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi. Ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nakushukuru kwa kuniona na pili kunipa nafasi niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kumekuwa na miito ya mara kwa mara viongozi wetu wa Halmashauri kuitwa na Serikali kwenda kujieleza au kupewa maagizo maalum: Je, hizi siku huwa zinahesabiwa kwenye siku 60, Kama hazihesabiwi kwenye hizo siku 60, haya malipo huwa yanatoka wapi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema, siku za nje ya kituo cha kazi. Kwa hiyo, zinaweza zikawa ni warsha, kongamano na kuitwa. Kwa hiyo, ni suala la mamlaka inayoidhinisha hizo safari kuangalia umuhimu wa hiyo safari ambayo mtumishi anakwenda kabla ya kuidhinisha. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali imetoa *circular* mara mbili juu ya kudhibiti mienendo mizima ya semina na warsha: Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kuliletea Bunge hili tathmini ya utekelezaji wa maagizo ya Serikali hasa tukizingatia kwamba kuna ongezeko kubwa sana la warsha na semina? Je, Waziri atakubali kabla ya Bunge hili kumalizika kutuletea tathmini sahihi kutokana na maagizo yale ya Serikali? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kipindi hiki ni cha bajeti na tuna maandalizi mengi sana, siwezi kumuahidi kwamba nitamletea tathmini kwa muda huu nilionao. Kwa kweli sina nafasi ya kufanya tathimini hiyo. Lakini kwa wakati mwingine tunaweza kufanya kwa maana ya kuangalia utekelezaji wa agizo hili la kuhusu warsha na makongamano.

**SPIKA**: Naona tuendelee. Lakini kabla sijamwita muuliza swali la tano Mheshimiwa Mabina, nilikuwa napenda kueleza kwamba mtaona Waheshimiwa Wabunge mezani kuna pipi. Ni sehemu tu ya maendeleo. Tunaposafiri kwenye mikutano mingi ya Kimataifa na kadhalika, hata hapa ndani hata hizo warsha mnazosema huwa kuna pipi.

Kwa hiyo tumeona ni jambo zuri la kuiga, kwa hiyo mchangamke. Lakini sharti lake ni kwamba unapouliza swali ama Waziri anapojibu swali asiwe anamung 'unya pipi. Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, swali la tano. *(Kicheko/Makofi)*

Na.5

**Malipo ya Wastaafu**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na matatizo ya wastaafu kupata malipo kidogo kutokana na kukokotoa malipo yao bila kuzingatia upandaji wa mara kwa mara wa gharama za maisha:-

Je, kwa nini Serikali isiwalipe wastaafu wote wanaopata kiwango cha shilingi 21,500, kiwango cha wafanyakazi wa kima cha chini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa viwango vya malipo ya pensheni vinavyolipwa kwa wastaafu nchini ni vidogo na havitoshelezi kukidhi mahitaji ya lazima ya wastaafu kutokana na tatizo la kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatambua na kuthamini mchango muhimu wa wastaafu wote nchini katika maendeleo ya Taifa hili kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kwa kutambua kupanda kwa gharama za maisha, Serikali imeendelea kuboresha viwango vya malipo ya pensheni mwaka hata mwaka kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai, 2003 Serikali iliongeza kima cha chini cha malipo ya pensheni kuwa Sh.21,601.05. Hata hivyo kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, Serikali inatambua kuwa kiwango hiki bado hakiwezi kukidhi mahitaji yao muhimu. Ndiyo maana Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, kwa mijadala na Miswada ya Sheria mbalimbali inayopitishwa, inaendelea kutafuta vyanzo zaidi vya mapato ili kuongeza mapato ya ndani na hatimaye kuleta maisha bora kwa Watanzania wote wakiwemo wazee wastaafu.

Aidha, Tume ya Rais ya Kuboresha Maslahi ya Watumishi iliangalia pia suala la pensheni. Hivi sasa Serikali inayafanyia kazi mapendekezo ya Tume ya Rais ya Mishahara iliyomaliza kazi yake mwezi Desemba, 2006. Lengo ni kuboresha viwango vya malipo ya watumishi pamoja na pensheni.

Mheshimiwa Spika, napenda ku1ihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa kadri tija itakavyoongezeka na pato la Taifa kuwa bora zaidi Serikali itaweza kutenga fungu la kulipa malipo ya pensheni kwa wastaafu wote kwa kiwango kinachokidhi mahitaji muhimu.

**MHE. ERNEST G MABINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wastaafu hawa wanapishana sana hasa ukiangalia marekebisho ya pensheni ya mwaka 1996 iliwaweka waliokuwa wastaafu kuanzia mwaka 1996 kupata malipo mazuri zaidi kuliko waliostaafu chini ya mwaka 1996; Je, Serikali ina mpango gani wa kuainisha uwiano huu na kuondoa tofauti iliyopo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wastaafu wanapishana kwa viwango vyao vya pensheni. Lakini hii inatokana na mishahara yao ya mwisho ambayo waliipata wakati wanastaafu. Kama nilivyotangulia kusema, ni kwamba Serikali inafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba wale ambao wanapata kima cha chini, basi kadri uchumi utakavyokuwa unaongezeka na wenyewe watakuwa wanaboreshewa pensheni yao. *(Makofi)*

**MHE**. **DR. WILBROD P. SLAA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa maslahi bora ya wastaafu wa sasa yanatokana na kazi nzuri waliyoifanya wastaafu waliopita, na kwa kuwa Sh. 21,500/= za sasa hazitoshi hata nusu ya matumizi ya mwezi. Je, Waziri atakubaliana kwamba sasa kuna sababu nzito zaidi ya kuhakikisha kwamba kila gharama za maisha zinapopanda basi na maslahi ya wastaafu pia yalingane na gharama hizo ili waweze kuishi maisha bora kama tunavyofanya sisi wastaafu wa leo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli gharama za maisha zinapanda lakini pia tunapoongeza mishara ya watumishi na hata pensheni za wastaafu tunaangalia na kasi ya

kukua kwa uchumi.

Kwa hiyo, napenda kuwahimiza wafanyakazi, wananchi kwa ujumla tujitahidi katika kukuza uchumi wetu. Uchumi ukiongezeka pato la taifa likiongezeka, basi maslahi ya watumishi pamoja na ya wastaafu yataweza kuboreshwa. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALl TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja baada ya majibu muafaka ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa ndani ya Tanzania kuna watumishi wa aina nyingi, lakini linaonekana hivi sasa kwa upande wa wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kama Kanali amestaafu mwaka 1980 na kuna mwingine amestaafu mwaka 1994 malipo yao ya pensheni yanakuwa hayana tofauti, na kutokana na hilo, yule aliyestaafu mwaka 1980 kwa mujibu wa kiwango chake cha mshahara anakuwa anapata kiwango cha chini. Kwa nini Serikali imeanzisha mtindo wa kulipa pensheni kwa wanajeshi kwa mkupuo badala ya utaratibu ambao upo hivi sasa? Je, kwa nini namba za pensheni mara nyingi huwa zinapotea? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMIHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, watumishi kama alivyosema kwamba wanatofautiana katika utumishi wa umma lakini pia utumishi katika vyombo vya ulinzi na usalama unatofautiana. Hata watumishi katika utumishi wa umma nao wako katika mifumo tofauti. Kwa hiyo, hata pensheni nazo zinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema namba za pensheni zinapotea. Suala la kutunza kumbukumbu sio la Serikali peke yake, ni suala 1a mwajiriwa na mwajiri ili kama pensheni itapotea kwa upande wa Serikali, basi yeye mwenye ile namba akiwa nayo atakuwa amesaidia Serikali. *(Makofi)*

**Na.6**

**Vyama vya Akiba na Mikopo kujenga Uwezo**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA (k.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kikao maalum kati ya Wabunge na Viongozi wa Benki ya *CRDB* na *NMB* kuhusu fedha za Serikali za kuwawezesha Wajasiriamali tarehe 16/04/2007 Dodoma, Uongozi wa *CRDB* ulikiri kuwa nyenzo za kuwezesha vyama vya akiba na mikopo kwa ukamilifu na kwa muda muafaka zina mipaka katika benki hiyo, na kwa kuwa, Serikali katika bajeti ya mwaka 2006/07 iliahidi kuvijengea uwezo vyama vya akiba na mikopo nchini ili kukidhi matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005:-

(a) Je, ni *SACCOs* ngapi na zipi zimeshafaidika kwa mpango huo wa Serikali mpaka sasa?

(b) Kama hazipo, Serikali ina mpango gani wa kutimiza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005-2010 inasisitiza dhana ya kuwajengea Watanzania utamaduni wa kujiwekea akiba. Kadri wananchi wanavyoanzisha *SACCOs* kwa madhumuni ya kuweka akiba kwanza na hatimaye kukopa wanatekeleza I1ani ya Chama Cha Mapinduzi. Uwezeshaji tunaouzungumzia katika maana hii, msingi wake ni kuweka akiba na shabaha ya kuwahimiza wananchi kuanzisha *SACCOs* na kama ilivyoainishwa kwenye Ilani, ni kuwajengea utamaduni Watanzania kuweka akiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba kumjibu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia Mei 31, 2007 nchi yetu ilikuwa na jumla ya *SACCOs* zilizoandikishwa 3,469.

Mafunzo kwa ajili ya *SACCOs* hizi yanatolewa na Asasi mbalimbali za Serikali na Asasi binafsi hapa nchini. Miongoni mwa Asasi za Serikali zinazotoa mafunzo hayo ni Idara ya Ushirika ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Mafunzo ya Biashara, Mradi wa *SELF*, Mradi wa *Rural Financial Services Programme* ambao unasaidia *SACCOs* na unaendeshwa katika Mikoa 10 hapa nchini ambayo ni Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Dodoma na Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Arusha, Manyara na Shinyanga, *SACCOs* hizo zinapata mafunzo kupitia mradi huo unaoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na kupata uhisani *wa IFAD.*

Aidha, Asasi binafsi inayoendesha mafunzo kwa *SACCOs* ni *Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania* (1992) *Limited kwa* kifupi *SCULLT.*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2007 hadi kufikia tarehe 1/6/2007 jumla ya viongozi watendaji wa Kamati wapatao 3,250 kutoka *SACCOs* 554 na jumla ya wanachama 157,800 kutoka SACCOs 669 wamekwishajengewa uwezo kupitia njia ya mafunzo. Aidha, Benki ya *CRDB* iliendelea kutoa mafunzo kwa *SACCOs* mbalimbali ambapo hadi sasa *SACCOs* zilizonufaika na mafunzo haya moja kwa moja kupitia utaratibu wa Benki ya *CRDB* ni 55.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia bajeti yake ya mwaka 2007/08 ambayo Waheshimiwa Wabunge mtapata fursa ya kuipitia na kuipitisha, inatarajia kutenga fedha za kuendesha mafunzo kwa SACCOs na wajasiriamali ili kuwajengea uwezo.

Fedha hizo zinatarajiwa kupitia Wizara ya Kilimo, Ushirika na Chakula, Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Pia Serikali kupitia Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kushirikiana

na Benki ya *NBC* imeanzisha mafunzo kwa wajasiriamali, ambapo miongoni mwa walengwa wa mafunzo hayo wamo viongozi wa *SACCOs.* Katika programu ya awali, mafunzo hayo yataendeshwa katika mikoa 12 ambapo jumla ya wajasiriamali 360 watanufaika na mafunzo hayo. Mikoa itakayonufaika na mafunzo kwa awamu ya kwanza ni Mara, Kagera, Kigoma, Shinyanga, Tabora, Mtwara, Lindi, Pwani, Rukwa, Morogoro, Singida na Dodoma.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Benki ya *CRDB* na *NMB* ambazo zimepewa jukumu la kutoa mikopo kwa ajili ya *SACCOs* na kwa kuwa benki hizi zimekuwa zikikatalia *SACCOs* ambazo ziko mbali na Makao Makuu ya Wilaya au Mikoa kama vile *SACCOs* ya Bukwimba, *SACCOs* ya UKIMWI imekataliwa; na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu mikopo hii ya *SACCOs* na wajasiriamali; je, Serikali iko tayari kubadilisha utaratibu badala ya kupeleka hizi pesa kupitia benki ya *NMB* na *CRDB* na kadhalika zipitie Halmashauri kama vile fedha MMEM, *TASAF* ili walengwa wapate kwa haraka na bila matatizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, hizi fedha zina awamu mbili, na jumla ya fedha hizi zilikuwa ni Shilingi bilioni 21. Awamu ya kwanza Shilingi bilioni 10.5 Serikali iliona ni vema kuzipitisha katika Benki hizi mbili ambazo zina mtandao mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba jambo hili la kuwawezesha wananchi la Shilingi bilioni 21 linafanyika kwa mara ya kwanza katika nchi yetu na ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Bila shaka kitu ambacho kinaanza kwa mara ya kwanza kitakuwa na matatizo yake ambayo kwa kawaida huwezi kuyatarajia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa inafanya tathmini na inaendelea kufanya tathmini kadri mikopo inavyoendelea kutolewa ili iweze kuja na utaratibu mzuri zaidi. Lakini kama ambavyo ilikuwa imeamuliwa hapo mwanzoni, Serikali ina mpango bado wa kuendelea kupitisha katika benki ili wananchi waweze kujenga tabia ya kuweka akiba, na hilo ndilo lengo kuu. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa hali ilivyo hadi sasa ni kwamba pamoja na Serikali kusisitiza mara kwa mara kwamba na wakulima wakopeshwe, lakini hakuna nia ya dhati kwa benki hizi kuwakopesha wakulima.

Pia uko ugumu mkubwa unaotokana na benki hizi kama *CRDB* kwa mfano, arnbayo ilikuwa imejikita kwenye kukopesha *SACCOs,* nyingi zimeshindwa kuchukua fedha hizo kwa sababu ya ukubwa wa riba na marejesho ya kila mwezi ambapo *SACCOs* haziwezi. Wakati wa kutoa kwenye *SELF* na *PRIDE*, *SACCOs* hizi zilikuwa zinachukua fedha na kurejeshwa kwa miezi mitatu au miezi sita na zaidi; Je, Serikali inasema nini juu ya matatizo haya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu hapo awali, Serikali inafahamu matatizo ambayo yameambatana na utaratibu huu mpya wa kuwawezesha wananchi. Nami ningezipongeza hizi benki kwa kazi ambazo wamezifanya mpaka sasa. *(Makofi)*

Kwa kweli wamefanya kazi kubwa, mpaka sasa wameshatoa karibu shilingi bilioni 17 kwa wajasiriamali mbalimbali hapa nchini na tufahamu Waheshimiwa

Wabunge benki duniani kote ni *conservative*. Utaratibu huu ni mpya, benki hizi zitabadilika kadri siku zinavyokwenda na utamaduni huu mpya ambao Serikali imeyapa jukumu mabenki haya kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati huu Serikali bado inaendelea kutathmini na mara kwa mara Serikali inaongea na benki hizi kurekebisha mwenendo ambao unaonekana unawakandamiza wananchi na unakwenda kinyume na zile Sera na Sheria ambazo benki hizi zimejiwekea.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *NMB* toka imeanzishwa majukumu yake yalikuwa siyo kukopesha wakulima. Serikali imeweza kuzungumza na *NMB* na sasa imekubali kuwakopesha wananchi. Hili ni jambo ambalo nafikiri ni zuri na linastahili pongezi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa laulau, pipi, ahsante sana. Kwa kuwa hizi ni fedha za wananchi maskini zinazotokana na kodi; na kwa kuwa Serikali hii ina mipango lukuki ambayo haiwezi ikatekelezeka kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, mamlaka ya kuweza kuweka hizi fedha katika hali ambayo ni ya mashaka mashaka, *risk area* imetoka wapi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana naye kwamba hizi kweli ni fedha za wananchi na wananchi maskini wanaolipa kodi na wanajitahidi sana kulipa kodi. Lakini pia sipendi kukubaliana naye kwamba mipango inasuasua kwa sababu ya bajeti. Mipango inatekelezwa kwa sababu mipango hiyo inawekwa kulingana na vipaumbele vya Serikali na kwa hivyo bajeti inavyopangwa, inapangwa kutokana na vipaumbele ambavyo vimewekwa. Kwa hiyo, sio rahisi mipango kusuasua kwa sababu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, ni Bunge hili ndilo ambalo linaidhinisha hiyo bajeti ya Serikali. Kwa upande wa wapi mamlaka hii imetoka, kwanza Serikali hii ni Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Ndiyo inatekeleza Ilani ya Chama ambacho kinatawala na katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi lipo bayana. *(Makofi)*

Ni kazi ya Serikali yoyote iliyoko madarakani kutekeleza zile Sera za Chama Cha Mapinduzi. Lakini la pili ni suala ambalo limeshajadiliwa hapa Bungeni na Wabunge wameshaliafiki. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja kwamba kwa kuwa mara nyingi benki hizi zipo kwenye miji mikubwa na vijiji vingi ambavyo vipo mbali na benki, mara nyingi vinapata taabu ya kukopa kwa sababu watu walioko karibu na miji ndio wanaoshughulikiwa zaidi; Je, kuna mpango gani kabambe uliopangwa sasa hivi ili na wale wa mbali, kwa mfano, katika vijiji vya Kipatimo, Njinjo na sehemu nyingine ambazo wao kusafiri kuja kwenye benki inawachukua muda mrefu na mpaka wengine hata hawajapata maendeleo, wanasikia kwenye redio tu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHA.JI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba mtandao wa benki hizi ambazo zimechaguliwa pamoja na kwamba ni mkubwa kuliko benki nyingine zozote ambazo tunazo hapa nchini, bado haufiki vijijini kama ambavyo tungetarajia. Benki ya *NMB* ambayo ina mtandao mkubwa zaidi ikijitahidi sana inafika kwenye

Wilaya na pengine kwenye Kata wana matawi mawili matatu.

Kwa hivyo, ni kweli kwamba wananchi watapata usumbufu katika kupata fedha hizi. Lakini mimi ningependa kutoa rai kwamba 1azima kwanza tuanze mahali.

Hata hivyo, wakati tunaanza, tulijua kwamba kutatokea matatizo ya umbali huu. Lakini ndiyo huo mtandao wa benki tulionao. Kwa hiyo, katika zile Shilingi billoni 10.5 zilipewa hizi benki. Lakini zile Shilingi billioni 10 zi1izobaki Benki Kuu na Serikali sasa hivi wanaandaa utaratibu mzuri zaidi wa kutumia Benki za Wananchi na *SACCOs* ambazo ni imara ili kuweza kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi.

Lakini pia katika maeneo mengine, wamefanya utaratibu wa kuweza kuwafikia hawa wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri na viongozi wa Kata. Wananchi wale wanajaza fomu zao zinapelekwa na Kiongozi wa Kata tu, anafika Benki kuuliza na kama fedha zao ziko tayari anakwenda kuwaarifu na wao wanasafiri wanakuja kuchukua fedha hizi ki1omita 100 nimeshaona wananchi wanaweza kupata misaada hii. Kwa hiyo, mimi ningetoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwasaidia wananchi katika kuwapa mawazo ili waweze kupata fedha hizi. *(Makofi)*

## Na.7

## Matatizo ya Maji Safi na Salama –Kigoma

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuiiza:-

Kwa kuwa kuna matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama katika Mji wa Kigoma:-

(a) Je, ni lini Serikali itaupatia mji wa Kigoma maji safi na salama?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mfupi na mrefu inayotekelezeka ya kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali lenye sehemu (a) na (b) la Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo kwa kuanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Kigoma - Ujiji ina wakazi wapatao 175,000 kulingana na sensa ya mwaka 2002 na watu wanaongezeka kwa asilimia 7.5 na inakadiriwa ifikapo mwaka 2020 watu wataongezeka na kufikia 797,000. Ongezeko kubwa la watu linatokana na wakimbizi wengi kutoka nchi za jirani wanaoingia Mkoani humo.

Mheshimiwa Spika, chanzo kikuu cha maji cha Manispaa hii ni Ziwa Tanganyika na mahitaji ya maji ni mita za ujazo 16,000 kwa siku ikilinganishwa na mita za ujazo 9,400 ambazo zinaweza kuzalishwa hivi sasa.

Mfumo wa majisafi uliopo ni wa siku nyingi na umechakaa na hivyo kutokidhi mahitaji ya maji hasa ikizingatiwa kuwa ongezeko la watu haliendi sambamba na upanuzi wa miundombinu. Huduma iliyopo sasa hivi inakidhi asilimia 50 tu ya mahitaji ya maji safi na salama. Aidha, katika Manispaa hii, hakuna mfumo wa maji taka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshirniwa Spika, Serikali ina mpango wa kuongeza huduma ya maji katika mji wa Kigoma/Ujiji kupitia *program* ya maendeleo ya Sekta ya Maji *(Water Sector Development Program)* kutoka asilimia 50 ya sasa hadi kufikia asilimia 75 ya mahitaji ifikapo mwaka 2010 kulingana na malengo ya MKUKUTA.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Wizara yangu imepanga kukarabati mradi wa maji wa mji wa Kigoma kwa kubadilisha mabomba chakavu, kufufua mitambo, kufunga mitambo mipya mitatu na kujenga *floating intake.* Ukarabati huu utateke1ezwa chini ya programu ya kuende1eza sekta ya maji. Jumla ya do1a za Kimarekani 1.45 milioni zitatumika kwa kazi hizi. Hatua hii itaimarisha upatikanaji wa maji katika mji wa Kigoma/ Ujiji

Mheshimiwa Spika, kupitia *Lake Tanganyika lntergrated Development Programme* inayofadhi1iwa na *Nordic Development Fund* Serikali ina mpango wa kuboresha huduma ya maji kwa mji wa Kigoma/ Ujiji. Kwa hivi sasa Serikali inapitia mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya usanifu wa mradi wa majisafi na majitaka.

Mheshimiwa Spika, mji wa Kigoma ni kati ya miji saba hapa nchini itakayonufaika na msaada wa fedha kutoka *EU Water Facility* kupitia Serikali ya Ujerumani: Jumla ya *Euro* 58 milioni zimetengwa kwa ajili ya kupanua huduma ya maji katika miji hiyo saba ikiwa ni pamoja na Kigoma. Kwa hivi sasa kiasi cha *Euro* 2.64 milioni zimetolewa kwa ajili ya upembuzi yakinifu, usanifu, na kuandaa makabrasha ya zabuni. Mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri unaendelea kwa sasa. Hivyo basi, utekelezaji wa mipango hii utahakikisha kuwa mji wa Kigoma/Ujiji unapata huduma ya maji ya kutosha.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ningeomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Mpango wa MKUKUTA ni kufikisha asilimia 75 ya maji kwenye Manispaa ya Kigoma inapofika 2010. Leo ni mwaka 2007, nilitaka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri sasa tumefika wapi? Hiyo asilimia kuanzia 50, tuko 55 tuko 60 tuko 62!

Swali la pili, mchakato wa kutafuta mzabuni unaendelea. Nilitaka kujua mchakato huu utakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa MKUKUTA umefikia wapi hadi sasa, ningependa kumsihi Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo ni kazi ambayo sitaweza kwa dakika hii hapa kuiongelea kwa sababu itabidi tuweze kupata takwimu za mikoa yote, wilaya zote, vijiji vyote ndipo hapo tunaweza tukampa jibu la uhakika. Kwa hali hiyo basi, naomba atupe muda na mimi nitampatia jibu hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa jibu la pili kuhusu mchakato wa kumpata mshauri, Mhandisi wa mradi ni kwamba kama nilivyomfahamisha kwamba hatua hiyo inaendelea, na katika kuendeleza hatua hiyo kuna masuala mbalimbali ambayo sifa za huyo mshauri zitaweza kutazamwa na hali kadhalika baada ya hapo ndipo itaweza kujulikana kwamba huyo Mshauri ndiye anayefaa na hiyo inachukua kipindi takriban cha zaidi ya hata miezi mitatu kwa kuwa siyo kazi ya kulipua ama sivyo tunaweza tukapata Mshauri ambaye anaweza akawa bomu tukashindwa kutekeleza kazi hiyo. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Sambamba na Mkoa wa Kigoma tuna tatizo katika Mkoa wa Lindi Wilaya ya Kilwa hususan katika vijiji vya Lihimalyao, Pande na Kijiji cha Ruyaya. Vijiji hivi havina maji kabisa. Je, Wizara inatamka nini kwa vijiji hivyo? Watapata maji lini? *(Makofi)*

**NAlBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maji kwamba kijiji gani kianze kupata maji na kipi kisipate maji, hilo ni jukumu la Halmashauri ya Wilaya wanapokaa ndipo wanaibua miradi ambayo inaletwa Wizarani kwa ajili ya kupewa maji. Nina uhakika kwamba sisi wote humu ndani tukiwa kama Madiwani ni jukumu letu na sisi kushiriki katika vikao hivyo na kuibua miradi ya Majimbo yanayotuhusu.

Kwa hali hiyo, naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi orodha hiyo ya vijiji ambavyo safari hii tumeletewa sinayo hapa, ila kwa sababu yeye ametaja vijiji vya Lihimalyao, Pande pamoja na Ruyaya, basi mimi nitakwenda kuhakiki kama vimo na kama havimo ningemshauri aibue miradi itakayofuata katika mradi huu wa maendeleo ya maji aweze na yeye kuhakikisha kwamba vinaingizwa katika orodha. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kuhusiana na swali la msingi ambalo Mheshimiwa Peter Serukamba ameliuliza. Wakati akijibu swali mwaka jana katika Bunge la Bajeti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji alisema kwamba katika Bajeti ya mwaka huu 2007/08 Serikali itaanza kutekeleza mradi kutokana na *Nordic Fund* kwa ajili ya mradi wa maji wa Manispaa ya Kigoma. Lakini alipokuwa anajibu swali la namna hiyo hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Peter Serukamba, leo Mheshimiwa Naibu Waziri ametaja miradi mitatu tofauti. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri awahakikishie wananchi wa Manispaa ya Kigoma ni mradi upi hasa ambao Serikali itautekeleza kwa kuhakikisha kwamba inaleta maji katika Manispaa ya Mji wa Kigoma. Ahsante.. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba katika jibu langu la mwaka jana, ni kweli kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba nilisema kuna mradi wa *Nordic Fund Development* ambao utatoa huduma ya maji pia Kigoma. Napenda kurudia kama ifuatavyo: Katika Mji wa Kigoma kuna miradi ya aina tano ambayo itahudumiwa, wa kwanza ni sisi wenyewe, Serikali yetu itahudumia. Kwa hivi sasa kuna mashine tano na mashine hizo tano za mradi wa maji na mashine hizo kwa sasa zinasuasua, hazifanyi kazi kwa sababu ni chakavu.

Serikali kwa sasa inashughulikia kununua mashine tatu kati ya tano ili kuhakikisha kwamba huduma ya maji inazidi kuboreka. Hilo la kwanza.

Pili ni kwamba, kuna huo mradi wa *Nordic Development Fund* ambao na wenyewe pia utaboresha huduma ya maji wa Mji wa Kigoma na tatu ni kwa kupitia *EU Water Facility* ambapo pia na yenyewe inatoa *Euro* rnilioni 58 kwa ajili ya kuhudumia

miji saba. Katika miji hiyo saba mojawapo ukiwa ni wa Kigoma na sasa hivi taratibu zimeanza kama nilivyoeleza ambapo *Euro* milioni 2.6 zimeanza kushughulikia makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.

Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hii miradi mitatu yote itasaidia katika kutoa huduma ya maji ya Mji wa Kigoma. *(Makofi)*

**Na.8**

**Tatizo la Maji Safi na Salama Muleba Kusini**

**MHE. WILSON M. MASILINGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Tarafa za Kimwani na Nshamba katika Wilaya ya Muleba zina watu wengi sana, 370,565 na zinakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama, hivyo kusababisha suluba kali kwa akina mama na watoto kutembea mwendo rnrefu kutafuta maji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Muleba kupata fedha za kugharimia miradi maalum katika Tarafa hizo hata ikibidi kutafuta Msaada toka kwa wafadhili?

(b) Kwa kuwa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuendeleza Makazi *(UN-HABITAT)* kwa ushirikiano na Serikali linatekeleza mradi wa maji safi na salama - Mji mdogo wa Muleba: Je, kwa nini fursa hiyo isitumike kuzipatia maji Kata za Bureza, Ikondo na Magata Karutanga ambazo ni jirani sana na mji huo na hasa ikitiliwa maanani kuwa umoja huo una uwezo mkubwa kifedha?

**SPIKA:** Naibu Waziri, 370,000 ni watu wengi. Kwa hiyo, ni sahihi tu, haibadili maana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, lenye vipenge1e (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Tarafa za Kimwani na Nshamba zina wakazi wengi na zina vijiji 61 kati ya vijiji 134 vilivyopo wi1ayani Muleba. Huduma ya maji iliyopo haikidhi mahitaji ya maji ya wakazi wa tarafa hizo. Kutokana na hali hiyo, Serikali hutenga fedha kwenye bajeti ya Wilaya ili kuendeleza huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali ilitenga Sh. 25,975,000/= kwa ajili ya kuchimba visima vifupi 10, katika vijiji vya Kabare visima viwili, Iramba kisima kimoja, Kakoma visima viwili, Nyakahenyei kisima kimoja, Kangantebe kisima kimoja, Ruhanga kisima kimoja, Mfumbo kisima kimoja na Bisore kisima kimoja.

Uteke1ezaji wa mradi huo upo katika hatua ya utafiti wa maeneo ya kuchimba

visima. Hata hivyo, kiasi kingine cha Sh. 12,600,000/= kimetengwa kwa ajili ya kukarabati mradi wa maji wa Kihwera ambao utanufaisha vijiji vya Kihwera na Mikale katika Tarafa ya Nshamba. Kazi ya ukarabati wa mradi inaendelea.

Aidha, kiasi cha Sh. 8,000,000/= kimetengwa kutoka katika ruzuku ya Serikali kwa ajili ya kukarabati mradi wa maji wa Nshamba. Kazi ya ukarabati wa mradi inaende1ea. Baada ya ukarabati kukamilika, vijiji vya Nshamba, Bunyagongo, Rutenge, Muzinga na Itongo vitapata huduma ya maji.

(b) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa maji katika mji mdogo wa Muleba unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuendeleza makazi *(UN-HABITAT)* umezingatia maombi yaliyopelekwa na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba na kukubaliwa.

Hivyo, kwa hatua iliyofikiwa sasa itakuwa ni vigumu kuingiza Kata za Bureza, Ikondo na Magata Karutanga kwenye mradi huo, kwa kuwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi zilikwishatengwa na Shirika hilo na utekelezaji wa mradi kwa mji wa Muleba umekwishaanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nimshukuru na kumpa hongera Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo yuko makini kufahamu huduma ya maji katika Jimbo lake na namshauri kwamba ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ili kubuni miradi mipya kwa ajili ya Tarafa za Kimwani na Nshamba na kuiweka kwenye mipango ya maji ya Wilaya ili iweze kutengewa fedha.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa na nampongeza pia yeye na Waziri wake kwa kazi nzuri wanayofanya kujaribu kutafuta fedha kwa ajili ya miradi ya maji katika nchi yetu. Nina maswali mawili.

Kwanza, kwa kuwa tatizo siyo miradi au uibuaji wa miradi, bali ni upungufu wa fedha katika bajeti ya Serikali yetu na ndiyo maana katika swali langu la msingi nilikuwa nashauri kama Serikali iko tayari kushirikiana na mimi kusaidiana kutafuta wafadhili ili tuweze kutekeleza miradi:-

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba bado ushauri huo ubaki pale pale ili tuweze kupata fedha nyingi zaidi badala ya fedha kidogo ambazo hata hazikidhi kukarabati miradi iliyobuniwa na kutekelezwa miaka ya 70 kwa mfano, katika eneo la Nshamba zimetengwa Shilingi milioni nane, hazitakamilisha eneo ambalo lina watu zaidi ya laki moja na nusu?

Pili, kwa kuwa maombi ya fedha kwenda Shirika 1a Umoja wa Mataifa katika majibu ya Serikali inaelezwa kwamba yalizingatia maombi ya Halmashauri ya Wilaya ambayo maombi yenyewe hayakuzingatia hali halisi ya mazingira ya Muleba, Kata ya Muleba au Tarafa ya Muleba:-

Je, Serikali itakubaliana na ushauri wangu kwamba ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba tukae pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa ambalo lina fedha nyingi sana ili kusahihisha makosa haya ya kitalaam yanayopelekea kuja kuwanyima wananchi wa Muleba au Tarafa ya Muleba maji safi na salama wakati fedha Umoja wa

Mataifa zipo na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ni Mtanzania na Katibu Mtendaji wa *(UN-HABITAT)* ni Mtanzania?

**SPIKA**: Nadhani inatosha. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji!

**NAIBU WAZIRI WAMAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha za Serikali zilizopo haziwezi kukidhi mahitaji ya maji ya nchi nzima kwa sababu tunafahamu maji ni kero kubwa.

Kwa hali hiyo basi, Mheshimiwa Mbunge ametoa ushauri kwamba tushirikiane naye kwa ajili ya kuweza kutafuta wafadhili ili waweze kutusaidia kukidhi mahitaji yetu ya maji, na mimi kwa niaba ya Waziri wangu wa Maji, nalipokea hilo kwa mikono miwili na tunamshukuru tuko tayari kufanya kazi naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, la kuhusu kwamba fedha za *UN Habitat,* hazikuzingatia hali halisi ya baadhi ya maeneo ikiwemo Wilaya ya Muleba na zaidi Muleba Kusini kwenye hizo Tarafa mbili na yeye alikuwa anapendekeza kwamba tuweze kukaa upya na kuyaangalia hayo masuala.

Mimi napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa hili la sasa kwa sababu mahesabu yameishafanywa, naomba tuliache liendelee isipokuwa kuanzia hapo miradi yoyote itakayohusika na kwa sababu miradi mingi tunaipitisha kwenye Halmashauri ninamwomba Mheshimiwa Mbunge pia ashirikiane na Halmashauri, kwa sababu sisi tunakuwa wa mwisho kupokea hiyo miradi.

Mheshimiwa Spika, hali halisi inafahamika kutokea kwenye Halmashauri na sisi pia tutakuwa makini kwamba miradi yoyote ya sehemu hiyo na kwa sababu tunajua hali ya maji ilivyo tutakuwa tayari kumfahamisha mapema Mheshimiwa Mbunge miradi itakayokuwa huko ili aweze kushirikiana na Halmashauri yake kuhakikisha kwamba Muleba inaingizwa katika programu hizo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kufidia muda nitaruhusu tuendelee kidogo. Mheshimiwa Michael Laizer umesimama mara nyingi sana, swali la nyongeza!

**MHE. MICHAEL L. LAlZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na miradi ya *Quick Winds* kwa nchi nzima katika Bajeti iliyopita, na sasa tunaingia kwenye Bajeti ya mwaka 2007/2008; Je, Serikali inawaambia nini wananchi katika miradi yote ya *Quick Winds* ambayo haikufanyika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna miradi inayoitwa *Quick Winds*, na nina uhakika kwamba kila Mheshimiwa Mbunge anaifahamu hiyo kwa kuwa Wizara yangu tulifanya semina kuhakikisha kwamba kila Mbunge anafahamu.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo siyo fedha zetu za nchini kusema kwamba Serikali ina hizo hela na inazitoa hapo kwa hapo. Ni miradi ambayo inategemea fedha za kutoka nje na miradi hiyo ni mojawapo ya miradi inayotegemea fedha kutoka *World Bank* na *African Development Bank.* Mchakato wa kushughulikia mpaka wafikie hatua

watoe fedha ni mambo ambayo yanapitia hatua mbalimbali.

Nakumbuka mara ya mwisho niliwafahamisha kwamba kwa upande wa fedha za *Quick Winds, African Development Bank*, tumeshafikishana nao hatua ya mwisho ili sasa tuweze kupata fedha na tunazitegemea fedha hizo wakati wowote.

Kwa hali hiyo basi, miradi ya ufadhili inategemea pia na wafadhili lini wanatoa fedha na lini tunazipata kuanza miradi. Hata hivyo, nina uhakika kwamba hatujachelelwa kwa sababu Halmashauri zote zimekuwa makini zikifanya michakato kwa miradi waliyoileta na pia wameleta marekebisho ya aina mbalimbali na wenyewe wamefikia hatua ambayo kwa sasa hivi wako tayari na fedha zitakapofika sasa hivi tutakuwa tayari kuanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba swali la mwisho la nyongeza na karibu sana kwa sababu umekuwa hospitalini kwa muda mrefu. Naona hali yako ni nzuri na tunakukaribisha tena ndani ya ukumbi huu. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, ninakushukuru sana na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuniombea. Bahati mbaya sana sijafika Jimboni kwangu, lakini nimerudi niko salama nadhani nitaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyoko Wilayani Muleba hayana tofauti sana na matatizo yaliyoko Geita. Shirika la *UN Habitat* limekuwa likitoa ahadi sana tangu mwaka 2002 na wananchi wamekuwa wakijulishwa.

Lakini utekelezaji wake wa kazi limekuwa likituchonganisha Waheshimiwa Wabunge ambao tumekuwa tukipeleka ujumbe kwa wananchi, kazi haifanyiki. Shirika linaahidi kujenga nyumba hazijengwi, shirika linaahidi kuleta maji, inakuwa ni tatizo kwa Muleba, Geita, Sengerema na Bunda na ramani zimeshachorwa muda mrefu, kazi hiyo haifanyiki.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu utekelezaji wa *UN Habitat* katika Wilaya za Geita, Bunda na Sengerema pamoja na Muleba utakuwa lini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *UN Habitat* wamekuwa wakichukua muda mrefu katika kutekeleza miradi na hii inatokana na taratibu zao mbalimbali ambazo sisi hatuwezi kuzilaumu.

Lakini hata hivyo, ni kwamba kwa kuwa ahadi yao wameitoa na sasa hivi wameshaanza kutekeleza miradi ya Muleba, kuna pia miradi ya Bukoba na pia watatekeleza mradi wa Mtukula upande wa Uganda na ambapo pia na upande wetu tutanufaika nao. Mimi nina uhakika kwamba tuvute subira na sehemu zingine zote kama walivyoahidi kiheshima watatufanyia hiyo kazi. Ni fedha ya kuomba na ni fedha ambayo inafuata taratibu zake.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali moja tu la Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwa hiyo, namuita muuliza swali Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali.

**Na.9**

**Ahadi ya Mashamba ya Kilimo cha Umwagiliaji –Mbarali**

**MHE. ESTHERINA J. KlLASI** a1iuIiza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Serikali iliahidi kuwaandalia wakulima wa Wilaya ya Mbarali hekta 10,000 za kilimo cha umwagiliaji ambazo hekta 3800 kati ya hizo zingeongezwa katika shamba la umwagiliaji la Mpunga lililoko Kata ya Madibira yenye ukubwa wa hekta 3000 kwa sasa:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika kutekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, Serikali imeweka mkakati gani katika kuhakikisha kuwa shamba hilo la umwagiliaji la Madibira linaendelea kutunzwa na wakulima kitaalamu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kumjibu Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Serikali iliahidi kuwaandalia wakulima wa Wilaya ya Mbarali walioonyesha nia ya kulima mashamba yaliyokuwa ya Serikali ya Kapunga na Mbarali ambayo kwa sasa yamebinafsishwa.

Katika kutekeleza ahadi hii Serikali imekwishakamilisha usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye skimu, Gwiri (hekta 500), Lwanyo (hekta 500) Uturo (hekta 700) na Kimani/Mbuyuni (hekta 1,000). Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji tayari imeanza katika skimu mbili za Uturo na Kimani na zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Ujenzi wa skimu zilizobaki umepangwa kuendelea kwa awamu kutegemea upatikanaji wa fedha. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maji

imekamilisha uchunguzi wa awali wa ujenzi wa bwawa katika Mto Ndembera. Ujenzi wa bwawa utawezesha hekta 3600 kuendelezwa kama awamu ya pili ya mradi wa Mabidibira.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu mkakati wa Serikali wa kuhakikisha shamba la Umwagiliaji la Madibira linaendelea kutunzwa na wakulima kitaalamu, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara imekwishaweka wataalamu wa fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na Maafisa Ugani na Mafundi Sanifu wa Umwagiliaji wanaosimamia uzalishaji wa mazao na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Wataalamu hao wanashirikiana na Chama cha Wakulima cha *MAMCOS*, Madibira *SACCOS* pamoja na Kamati mbalimbali za uendeshaji wa skimu ya Madibira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Estherina Kilasi, swali la nyongeza na ndilo la mwisho.

**MHE. ESTHERINA J. KlLASI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza na ninampongeza Naibu Waziri kwa maana ndiyo ameanza katika Wizara hii kwa jibu lake zuri kwa sehemu ya kwanza.

Sehemu ya pili, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikipunguza watumishi wa Mradi wa Umwagiliaji wa Madibira na hadi hivi sasa ninavyoongea kuna watumishi watano tu waliobaki na wengine ni wa shughuli zingine tofauti na hizo alizozitaja na ni mmoja tu ndiye anayeshughulikia mambo ya kilimo; na kwa kuwa hali ya mradi huu ni mbaya sana kimazingira, maeneo ya majengo yenyewe mradi ulipokuwepo na miundombinu ya shamba imekuwa ikiharibika siku hadi siku, na mpango wa Serikali ulikuwa mara nyingi kwa watumishi wa mradi kutafuta nyenzo kama matrekta na hatimaye kuwakodisha wakulima wanaolima ndani ya mradi huo.

Je, mradi huo wa umwagiliaji tayari uko chini ya Ushirika wa Wakulima wa Kata ya Madibira au bado unasimamiwa na Serikali ili baadaye isije ikawa hatma kwa wakulima kwamba wameshindwa kutunza mradi huo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mradi huu sasa hivi kuna maeneo ambayo yameshafanyiwa usanifu na mengine ambayo yameshaanza ujenzi. Niseme kwamba mradi huu unapokamilika ndipo wananchi watakapokabidhiwa.

Lakini kwa sasa hivi kwa sababu bado tuko kwenye hatua hizi za ujenzi na zingine kwenye usanifu bado hawajakabidhiwa.

**SPlKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Swali moja lililobaki tutaweza kulishughulikia kesho ama siku nyingine.

Nina matangazo machache tu. Kwanza, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami (Mbunge),

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ameniomba niwatambulishe wageni wake kutoka Moshi Vijijini, Jimboni kwake ambao wanaongozwa na Mama Joyce Austin na wapo kwenye *gallery* pale. Naomba msimame ni hao wanne. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mwalimu Msaidizi wa *Bunge Sports Club* anawakumbusha wanamichezo wote Waheshimiwa Wabunge kwamba mazoezi yataanza kesho alfajiri kama kawaida, usafiri upo na utapita katika maeneo yenu kuanzia saa 11.00 alfajiri. Wanamichezo basi wajue hali hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa taratibu za Mkutano wa Bajeti, leo Shughuli zeto zinaishia na kipindi hiki cha Maswali na Majibu kwa Kikao cha leo na kesho vile vile ni kipindi cha Maswali na Majibu tu. Ila leo baada ya kipindi cha maswali na nikishaahirisha Shughuli za Bunge tutafanya kikao cha *briefing* katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Waziri Mkuu amenihakikishia kuwa atakuwa kwenye kiti saa 4.30. Kwa hiyo, ninawaomba kama ni kusalimiana labda baada ya hapo ili tuweze kuzingatia mambo mbalimbali yanayohusika na Mkutano mzima huu wa Nane wa Bunge. Kwa hiyo, saa 4.30 *briefing* kwa Waheshimiwa Wabunge wote pale Ukumbi wa Pius Msekwa.

Kwa nafasi hii nitangaze tu zile *caucus* za vyama ni kadri ambavyo Makatibu watajipangia mathalani mchana leo au hata kesho. Kwa sababu nafasi ipo. Hayo ndiyo matangazo niliyoyapata.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naomba sasa kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu Asubuhi.

(*Saa* 4.15 *Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe* 13 *Juni, 2007)*